

# Raka'āh 20 za Taraweeh

Hazrat Atā bin Abi Rabah (aliyefariki mwaka 114 A.H), ambaye ni Tabi'i, alikuwa Mufti wa Makkah Mukarramah. Anasimulia kuhusu mwenendo na tabia ya watu wa zama zake (yaani masahabah na Tabi'in) huko Makka Mukarramah: "Niliwakuta watu wakiswali Raka'ah 23." (20 za Taraweeh + 3 za Witri)

(Musannaf ibn Abī Shaybah 7770)

